مجلة العلوم الإنسانية
Journal of Human Sciences
www.Suj.sebhau.edu.ly
Received 12/09/2016 Revised 05/06/2017 Published online 04/07/2017

# UTAYARISHAJI WA VITABU VYA KISWAHILI NCHINI LIBYA

IBRAHIM ELHADI MOHAMED
IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA KIAFRIKA,KITIVU CHA SANAA,CHUO KIKUU CHA SEBHA,Libya

**MUHTASARI**
Makala haya yamejadili suala la utayarishaji wa vitabu vya Kiswahili nchini Libya, Katika makala haya tumetoa taarifa kuhusu misingi ya Utayarishaji na Uandishi wa Vitabu vya Kiada, aidha tumechunguza hali ya Uandishi nchini Libya kwa Jumla. Hali kadhalika hali ya Uandishi wa Vtabu vya Kiswahili Nchini Libya umejadiliwa kwa kina.

**الملخص**
تناقش هذه المقالة قضية اعداد كتب للغة السواحلية في ليبيا. وقد تطرق الباحث الى الأسس والمبادى الأساسية المتبعة في اعداد وكتابة الكتب المنهجية بصورة عامة كما تناول الباحث وضع التأليف ومسيرته خلال الفترة السابقة . قام الباحث بمناقشة وايضاح الحالة التي يمر بها اعداد الكتب المنهجية للغة السواحلية في ليبيا بصورة خاصة وبيان ماوصلت اليه.

**UTANGULIZI**
Nchini Libya, kuna waandishi na watunzi wa vitabu vinavyoelezea taaluma mbalimbali na kuandikwa kwa lugha mbalimbali (Kiarabu, Kihausa, Kifaransa, Kiingereza,..), vikiwemo vitabu vya Kiswahili. Ingefaa tudokeze hapa kwamba mbali na lugha nyingine tulizotaja hapo juu, hii ni mara ya kwanza kabisa katika historia ya Elimu ya Walibya kuzungumzia uandishi na uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili.
Wengi wameandika kuhusu vitabu vya kiada vya Kiswahili, hususani katika shule za msingi na upili lakini je, nini kuhusu uandishi wa vitabu vya kiswahil nchini Libya?

**Misingi ya Uandishi wa Vitabu vya Kiada**
Uandishi wa vitabu huchangia pakubwa katika kufanikisha malengo ya elimu katika nchi yoyote iwayo. Mbunda (1983: 16) anasema:
''Kazi ya uandishi ni kazi ngumu sana. Inahitaji kuhusisha vyombo vingi sana vya Serikali na siasa yake, walimu, wataalamu, wazazi na hata wanafunzi wenyewe. Uamuzi wa uandishi si wa mtu mmoja, ni wa mfumo mzima wa wale wanaohusika'.
Mayoka (2003:55 ), anasema:

> *"uandishi ni sanaa ya kuzua mawazo, fikira, ujuzi na maarifa na ni ya sayansi ya kuyawasilisha mawazo yetu kwa maandishi."*

Mbunda (1987) anasema kuwa kuna misingi ipasayo kufuatwa katika uandishi wa vitabu vya kiada. Ameorodhesha misingi na fafanuzi zake. Tumeona bora kuiweka bayana katika kazi hii kama ifuatavyo:

**1- VITABU VYA KIADA VIWE NA LENGO KWA WALE WATAKAOHUSIKA**

Ufundishaji darasani unategemea sana vitabu vya kiada. Kwanza, vinamsaidia mwalimu iwapo yeye mwenyewe hana ujuzi mkubwa wa somo alifundishalo. Vitabu vya aina hii vitakuwa marejeo yake ya mara kwa mara katika somo au masomo ayafundishayo. Pili, vitabu vya kiada ni msaada mkubwa kwa mwanafunzi katika kujifunza kwa mpango maalumu, katika kujipima, kufanya marudio, na pia katika mafunzo ya ngazi ya juu. Kufaa kwa vitabu vya kiada ni suala la msingi kabisa katika uandishi wake.
Tukimwangalia mwanafunzi, kwanza tutaona kuwa ana mahitaji na matakwa yake. Mahitaji yake yatalingana na yale ambayo taifa lake linataka awe nayo, na matakwa yake yatafuatana na mwelekeo wake binafsi. Aidha katika kusisitizia mahitaji na matakwa ya mwanafunzi tunapambana na matatizo ya muundo na msamiati mgumu kwa wakati mmoja. Suluhisho ni kwamba tutumie msamiati mgumu katika muundo mwepesi, na msamiati mwepesi katika muundo mgumu.
Uandishi wa vitabu vya kiada lazima uhusishe pia walimu watakaofundisha masomo hayo. Walimu hao watafikiriwa katika pande mbili: Kwanza, kuwepo kwao, na pili, ujuzi wao katika somo lihusikanalo. Ulikuwepo wakati ambapo nchi hii iliunda muhtasari na kuandaa vitabu vyake vya kiada kwa somo la Kiingereza katika shule za msingi bila kufikiria pande hizo mbili za walimu. Ingawaje palifanyika semina za dharura, matokeo yake hayakufanikiwa sana.
Ni muhimu basi, katika uandishi wa vitabu vya kiada kuwafikiria wale watakaohusika na vitabu hivyo; yaani wanafunzi katika kutimiza mahitaji na matakwa yao, na kisha walimu, iwapo wapo wa kutosha na wana ujuzi wa somo lishughulikiwalo.

**2- VITABU VYA KIADA VIANDIKWE KULINGANA NA MALENGO YA ELIMU**

Taifa lolote lile sharti liwe na shabaha zake katika kuendeleza raia wake. Njia mojawapo kuu katika kutekeleza malengo na shabaha za taifa ni katika utoaji wa elimu. Sehemu muhimu ya shughuli hiyo hufanyika shuleni na vyuoni. Nako huko mambo mengi yatolewayo yamo vitabuni, na baadhi ya hivyo vitabu ni vya kiada. Hivyo basi, iwapo tunataka kuwajenga raia katika mfumo fulani wa maisha hapana budi vitabu vitumikavyo shuleni na vyuoni vilingane na msimamo wa taifa linalohusika. Kila nchi, na kila taifa lina malengo yake katika mfumo wake wa elimu.
Kobia, J. ( 2006), anadai wamba umuhimu wa kuzingatia malengo ya taifa katika uandishi wa vitabu vya kiada utaonekana katika jinsi taifa hilo linavyoichukulia elimu. Tukiamini kuwa elimu ni

nyenzo muhimu ya maisha na maendeleo, nadhani hatutaliachilia mbali suala hili la kuingiza malengo ya taifa katika vitabu tuandikavyo na kuchapisha.

**3- UANDISHI WA VITABU VYA KIADA UTOKANE NA MUHTASARI ULIOKWISHA KUANDALIWA**

Besha, M.R. (1978) alieleza kwamba utaratibu unaopaswa kufuatwa ni kwamba kwanza nchi itoe uamuzi kuhusu malengo yake ya elimu. Pili, unatengenezwa muhtasari ili kutekeleza malengo hayo. Tatu, vinaandikwa vitabu kufuatana na muhtasari huo. Kwa kawaida vitabu vya kiada hutokea kwanza vikifuatiwa na vile vya ziada.

Muhtasari kwanza unaonesha madhumuni ya ufundishaji wa somo lolote lile, pili, nini kifundishwe na kwa utaratibu gani. Hivyo waandishi wa vitabu hufuata kila sehemu ya yaliyomo katika muhtasari. Ni wazi kuwa muhtasari utakuwa na idadi fulani ya mambo ya kufundisha kufuatana na somo au madarasa. Kila jambo linalotarajiwa kufundishwa hugawanyika tena katika sehemu ndogondogo, nazo huwa zimepangwa kwa utaratibu wake. Kwa kawaida utaratibu huo ni mfululizo wa mada zinazoanzia na mambo rahisi, hadi kufikia magumu; yanayojulikana hadi kufikia yasiyojulikana ; na mambo mepesi hadi kufikia mazito.

Vitabu sharti viandikwe kwa kufuata utaratibu huohuo wa muhtasari, yaani vianze ngazi ya chini na kuendelea hadi ya juu. Hali hii ni katika kulifikiria somo, na hali kadhalika madarasa. Katika shule za msingi au za sekondari, na hata vyuo vikuu, vitabu viandikwe kwa ngazi zake; itakuwa vigumu kufanikisha vitabu vya kiada iwapo vitaanzia juu katika uandishi wake hadi kufikia ngazi ya mwanzo. Msingi huu wa uandishi wa vitabu vya kiada unasisitiza kuufuata muhtasari na utaratibu uliomo.

4- **SHUGHULI ZA UANDISHI WA VITABU VYA KIADA ZIWE THABITI**

Uandishi wa vitabu ni shughuli ambayo ipo daima. Uandishi wa vitabu waweza kuwa wa mtu binafsi au wa kundi la watu. Uandishi wa vitabu vya kiada hapa Libya umejumuisha aina zote mbili za waandishi, yaani binafsi na wale wa vikundi.

Katika kufanikisha uandishi wa vitabu vya kiada kuna mambo kadhaa ya kuangalia. Kwanza, lazima pawepo na sababu ya msingi ya uandishi huo, kwa mfano, mabadiliko katika siasa ya nchi, kutokufaa kwa vitabu vya zamani ( baada ya utafiti wa kina), taaluma mpya imeingizwa katika muhtasari, au kuwepo kwa upungufu mkubwa katika vitabu vilivyopo.

Pili, pawepo na tamko rasmi kuhusu uandishi wa vitabu hivyo. Kwa kawaida iwapo muhtasari umekwishakuundwa patakuwepo pia na mapendekezo ya vitabu vitakavyotakiwa kuambatana na muhtasari huo, iwe vitabu hivyo vipo au havipo. Kama havipo, basi patakuwa na haja ya kuwa na vitabu hivyo. Mara nyingi tamko namna hii hutolewa na chombo cha juu kabisa katika nchi, nacho ni wizara inayohusika. Tatu, pana haja ya kuamua ni nani watahusika katika shughuli hiyo ya uandishi, kama ni mtu binafsi au ni kikundi cha watu.

**5- VITABU VYA KIADA VIWE NA LENGO LA KUMWENDELEZA MWANAFUNZI BINAFSI**

Haji, A.I. (1983), anasema kwamba Elimu katika nchi yoyote ni ya kumwendeleza binadamu, hivyo, hata vitabu vitumiwavyo kutolea elimu havina budi kukidhi haja hiyo. Shuleni au vyuoni wanafunzi husomea somo fulani kwa muda wa miaka kadhaa. Tunachotegemea ni kuwa wanafunzi hao watapanuka kielimu na kimaarifa. Hivyo, iwapo pana mfululizo wa vitabu vya kiada katika somo moja, vitabu hivyo vitokane na msingi wa vitabu vilivyotangulia. Yaliyomo katika kitabu cha kwanza yaendelee katika kitabu cha pili na cha tatu, lakini kwa viwango zaidi. Kwa njia hii msingi utaendelezwa katika utaratibu uleule bila kupoteza kitu, na mwanafunzi hata kama atajisomea mwenyewe hatakuwa na tatizo sana katika kuyafuata yaliyomo kutokana na uhusiano uliopo kutoka kitabu kimoja hadi kitabu kingine.

Kumwendeleza mwanafunzi binafsi hakufikiriwi katika kupanua maarifa na kuendeleza stadi tu. Katika lugha, kwa mfano, tunafikiria pia wajibu wa kuzuia na kurekebisha makosa. Kwa hiyo, vitabu vya kiada vya lugha vina sura au hupaswa kuwa na sura kadhaa ambazo hazina jambo geni, ila kusisitiza yaliyopita na kutoa fununu ya yatakayokuja.

Kwa kifupi basi, maarifa na stadi zinazoanzishwa katika kitabu cha kwanza ziendelee katika vitabu vifuatavyo vikihusishwa na viwango vya wanafunzi. Hali kadhalika pawepo na nafasi ya kumsaidia mwanafunzi katika kupambana na matatizo ambayo anapaswa kukabiliana nayo.

**HALI HALISI YA UANDISHI NCHINI LIBYA**

Hali halisi ya uandishi nchini Libya bado ni tatanishi. Algalaal (1994 :8) katika kitabu chake alieleza kwamba uandishi nchini Libya umeanza mwaka 1953 na waandishi walikuwa wachache sana. Ameongeza kusema kwamba ijapokuwa imepita takribani miaka sitini, vitabu ambavyo vimeandikwa ni kati ya elfu thelathini na tano (35,000) na elfu arubaini (40,000).

Alhawat , Alawami & Said (2004) Uandishi wa vitabu vya vyuo nchini Libya, umeanza mwaka 1967. Waandishi na wachapishaji wa vitabu vya vyuo waliohudhuria semina ya uchapishaji wa vitabu vya vyuo nchini Libya iliyoendeshwa katika Chuo Kikuu cha Garyunis, walihitimisha kwamba baadhi ya matatizo makubwa na vizuizi vinavyochangia katika upungufu wa idadi ya vitabu vya vyuo ni kukosekana kwa vyanzo vya taarifa. Waandishi hawaoni umuhimu wa kuhudhuria mikutano ya kielimu pamoja na kwamba hawapati maslahi makubwa yanayohusu utungaji wa vitabu vya vyuo. Waliohudhuria semina hiyo walihitilafiana kuhusu idadi ya anwani za vitabu vya vyuo vilivyochapishwa katika miaka arubaini na tano (45) iliyopita, kama ni elfu nane (8,000) au elfu kumi (10,000); lakini wote walikiri kwa pamoja kwamba vitabu vya vyuo bado ni vichache mno.

**HALI HALISI YA UANDISHI WA VITABU VYA KIADA VYA KISWAHILI NCHINI LIBYA**

Uamuzi wa kukifundisha Kiswahili nchini Libya ulifikiwa mwaka 1984. Kutokana na uamuzi huu

kukawa na haja ya kuandika vitabu vya kiada vya Kiswahili nchini Libya.

Katika kufanikisha lengo tajwa hapo juu, Wizara ya Elimu ilianza kutekeleza majukumu hayo: mojawapo ni la kuandika vitabu vya kiada vya Kiswahili katika ngazi za Shule za Upili na Vyuo Vikuu. Haukupita muda, takriban kama miaka kumi na sita, wakajitokeza waandishi mbalimbali walioviandika vitabu hivyo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya sekondari, vyuo vikuu na elimu ya juu nchini Libya ili kuliziba pengo liliopo.

Ijapokuwa imepita zaidi ya miaka thelathini na tatu (35) tangu uamuzi wa kukifundisha Kiswahili uanze nchini Libya, imebainika kwamba idadi ya Vitabu vya Kiswahili vilivyoandikwa nchini humu bado ni ndogo. Ifuatayo ni orodha ya vitabu vya Kiswahili vilivyoandikwa nchini Libya kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka 2017 ambavyo ni ushahidi mmojawapo wa kuonesha uchache wa vitabu vya kiada tangu uamuzi wa kukifundisha Kiswahili utangazwe mwaka 1984:

**1- Vitabu ambavyo tayari vilichapishwa:**

| Na. | Jina la kitabu | Jina la mwandishi | Mwaka | Mchapishaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Sarufi Miundo ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 2. | Sarufi Maumbo ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 3. | Fonetiki Matamshi ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 4. | Vitenzi na Majina ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 5. | Matumizi ya Lugha | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 6. | Karibu Tuongee | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 7. | Upatanisho wa Vivumishi na Majina ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 8. | Misingi ya Sarufi ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 9. | Sarufi Tangulizi ya Kiswahili (Sarufi Maumbo) | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 10. | Misingi ya Sarufi ya Kiswahili | Prof. E. Wesana Chomi | [2005] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 11. | Kiswahili kwa Libya: Daraja la 1, shule za Maandalizi | Prof. E. Wesana Chomi na Othman Abdulsalam | [2000] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 12. | Kiswahili kwa Libya: Daraja la 2 shule za Maandalizi | Prof. E. Wesana Chomi na Othman Abdulsalam | [2000] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 13. | Kiswahili kwa Libya: Daraja la 3 shule za Maandalizi | Prof. E. Wesana Chomi na Othman Abdulsalam | [2000] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 14. | Sarufi 1 Shule za Sekondari | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2007] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 15. | Ufahamu 1 Shule za Sekondari | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2007] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 16. | Mazungumzo 1 Shule za Sekondari | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2007] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 17. | Maabara ya Lugha 1 Shule za Sekondari | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2007] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 18 | Kusoma na Kuandika 1 Shule za Sekondari | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2007] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 19 | Matamshi 1 Shule za Sekondari | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2007] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 20 | Misingi ya Kiswahili | Dkt. Idriss Hasan | [2007] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 21 | Tuanze Kusoma | Dkt. Idriss Hasan | [2008] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 22 | Nyanja Linganishi za Fonetiki ya Kiswahili na Kiarabu | Ibrahim Elhadi Mohamed | [2008] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 23 | Mfanano wa Methali za Libya na Tanzania | Ahmeda Al Sanosi | [2008] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 24 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 2A Kitabu cha Mwanafunzi | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2008] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 25 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 2B Kitabu cha Mwanafunzi | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2008] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 26 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 2A na 2B Kitabu cha Mazoezi | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2008] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 27 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 2A na 2B Kitabu cha Mwalimu | Dkt. Abubaker Oheda na Ibrahim Elhadi Mohamed | [2008] | Wizara ya Elimu nchini Libya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 28 | Kiswahili | Dkt. Othman Abdulsalam na Dkt. Abubaker Oheda | [2002] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 29 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 3A Kitabu cha Mwanafunzi | Prof. E. Wesana Chomi na Othman Abdulsalam | [2009] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 30 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 3B Kitabu cha Mwanafunzi | Prof. E. Wesana Chomi | [2009] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 31 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 3A na 3B Kitabu cha Mazoezi | Prof. E. Wesana Chomi | [2009] | Wizara ya Elimu nchini Libya |
| 32 | Kiswahili kwa Walibya: Shule za Sekondari 3A na 3B Kitabu cha Mwalimu | Prof. E. Wesana Chomi | [2009] | Wizara ya Elimu nchini Libya |

**2- Vitabu ambavyo baado havijachapicwa:**

| **Na.** | **Jina la kitabu** | **MWANDISHI** | **MWAKA** | **MCHAPISHAJI** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ( الجملة السواحيلية البسيطة الخبرية ) | Dkt . Ahmeda Al Sanosi | [2015] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 2. | Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kondoro: mifano kutoka katika mashairi yake. | Dkt . Mohamed Yunis | [2016] | Chuo Kikuu Cha Sebha |
| 3. | Lugha Ombya | Dkt . Salim Mahmud | [2016] | Chuo Kikuu Cha Sebha |

**HITIMISHO**

Katika makala haya tumeona kwamba vitabu vya Kiswahili ni muhimu sana kwa uenaji, ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya kiswahili nchini Libya. Kwa hiyo hapana shaka kwamba vitabu bora vitakuwa msaada muhimu sana kwa ufundishaji bora pia.

Kutokana na taarifa iliyotajwa hapo juu, tumeona kwamba Vitabu vya Kiada vya Kiswahili ambavyo vimeandikwa nchini Libya ni vichache mno na maudhui yake ni finyu mno kwa walengwa, hususani wanafunzi wa vyuo vikuu.

**Mapendekezo**

Ili kuboresha hali ya uandishi wa vitabu vya kiada vya Kiswahili nchini Libya tunatoa mapendekezo yafuatayo:

1. Semina kwa ajili ya Waandishi ziwe zinaendeshwa mara kwa mara na Wizara na asasi zinazohusika.
2. Kuanzishwe na kuendeshwe Jarida la Kiswahili nchini Libya.
3. Waandishi wa vitabu vya Kiswahili hawana budi kujibidiisha kufanya utafiti wa kina kabla ya kuandika vitabu vyao ili waweze kutoa vitabu bora vitakavyotumiwa nchini Libya.
4. Marejeo muhimu yangepatikana pasingekuwa na tatizo kubwa kwa waandishi wa Vitabu vya Kiswahili.
5. Vitabu vya Kiada lazima vitathminiwe na wataalamu wanaoshughulikia masuala ya kutathmini vitabu.
6. Waandishi wanatakiwa kuelewa malengo yao, hususani kuhusu hadhira, wakati wa kutayarisha vitabu vya kiada.
7. Kuendeshwe warsha za mara kwa mara za uandishi wa vitabu ili kuboresha vitabu vilivyochapishwa, hususani kimaudhui.

**MAREJELEO**

[1]- Algalaal ( 1994 ) الناشرون ونشر المطبوعات منشورات احمد محمد القلال 1994 ) جامعة قاريونس

[2]- Alhawat , Alawami & Said (2004) على الهادى الحوات ( 2004+ /) عبدالعالى العوامى / د. بشير احمد سعيد محمد مسيرة التعليم العالى فى ليبيا انجازات وطموحات النقابة العامة لاعضاء هيئة التدريس الجامعى

[3]- Besha, M.R. (1978), "Utayarishaji wa Vitabu vya Kufunzia Wageni Kiswahili", *katika* Semina ya Kimataifa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

[4]- Haji, A.I. (1983), Jinsi ya Kuandaa Somo la Sarufi ya Kiswahili kwa Wageni. *katika Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili* : Uandishi na Uchapishaji. Dar es Salaam. TUKI.

[5]- Kobia, J. ( 2006), Matatizo Yanayowakumba Waandishi wa Vitabu vya Kiswahili Nchini Kenya, *katika* Nordic Journal of African Studies 15(2), 2006.

[6]- Mayoka, J.M.M. (1983) Utayarishaji na Uandishi wa Vitabu vya Elimu ya Watu Wazima.

[7]- Mbunda, F. (1983), Misingi ya Uandishi wa Vitabu vya Kiada, *katika Makala za semina Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*: Uandishi na Uchapishaji. Dar es Salaam. TUKI.

[8]- Mbunda, F. L. (1978),Ukusanyaji wa Data ya Mswada hadi kuwa kitabu.